Ninawezaje Kumpata Mungu?

na

Ellis P Forsman

(How Can I Find God?)

Ninawezaje Kumpata Mungu?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12,2011

Ninawezaje Kumpata Mungu?

Ayubu 23:3

Ayubu 23:3, "*Laiti ningejua mahali niwezapo kumwona, nifike hata hapo anapokaa.*"

Chini kpitia kilio cha Ayubu. Kilaa wakati Ayubu alikuwa mtu wa Mungu, lakini kwa sababu ya Shetani kumsumbua kwa misiba na mateso, alimtafuta Mungu kwa machungu ya moyoni. Alidhani kwamba Mungu alimwacha na hivyo akataka kumtafuta.

Mara nyingi watu wamekuwa wakimtafuta Mungu.

Wengi wanadai hawawezi kumpata. Wanauliza, "Ninawezaje Kumpata Mungu?"

Swali hili ni muhimu sana. Pia ni mapenzi ya Yesu Kristo kwamba Mungu apatikane.

Yoh. 17:3, "*Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.*"

Kujibu swali hili, "Ninawezaje Kumpata Mungu?" ni muhimu sana.

Ebu na tujifunze swali hili, "Ninawezaje kumpata Mungu?" wengine wanadhana mbaya katika kujaribu kumtafuta Mungu.

Jinsi wengine wanavyojaribu kumtafuta Mungu.

Kiasili.

Wapo wale wwanaomtazama Mungu kwa asili – hiyo inaitwa wasio na imani. Wanaamini kwamba Mungu anakaa kwenye miti, nyota, mwezi, nk. Mila nyingi duniani wanaimani hizi katika Mungu. Wamarekani wa Kihindi wa kwanza nao pia waliamini hili pia; kwamba kulikuwa na miungu mingiambao waliishi kwenye ndege, wanyama, nyota, jua, nk.

Kwa binadamu.

Wapo wale wanaoamini kwamba binadamu ni mungu wake mwenyewe; na kwamba binadamu wote ni miungu yao wenyewe. Huu unaitwa ubinadamu. Hawaamini katika baada ya maisha; hivyo wanaishi kukidhi hamu yao wenyewe, kuishi kwa kuufuata mwili.

Katika fumbo na ibada.

Wapo wale wanaomtafuta Mungu katika mafumbo na ibada. Ni Mungu asiyejulikana kwa wengi.

Mdo. 17:21-31, "*Kwa maana Waathene na wageni waliokaa huko walikuwa hawana nafasi kwa neno lolote ila kutoa habari na kusikiliza habari za jambo jipya. Paulo akasimama katikati ya*

Areopago, akasema enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini. Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi mimi nawahubiri habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye kwwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote, kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mtu mmoja wakae juu ya uso wan chi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu mtunga mashairi alivyosema, maana sisi sote tu wazao wake. Basi kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu na fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu. Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu."

Wengine hawataki kimtafuta kabisa.

Wengine wanatabia ya, "Siwezi kujali" au "Naweza kufanya shughuli bila hata yeye."

Kama wakiishi maisha yao yote na tabia hizo, siku ya hukumu itaenda kuwa yenye kuwashtua; alafu muda utakuwa umeisha.

Kwa nini tunahitaji kumtafuta (na kumfahamu) Mungu

Sababu moja ni kwa sababu ya kile anachoweza kutufanyia katika maisha haya. Anaweza kutusaidia kukabiliana na matatizzo yetu ya shauku, mizigo, uchungu, huzuni, nk. Hayupo mfariji mkuu kuliko kufahamu kwamba Mungu yupo kutusaaidia.

- Yakobo 5:13, "*Mtu wa kwenu amepatikana na mabaya? Na aombe, ana moyo wa kuchangamka? Na aimbe zaburi.*
- 1 Nyak. 16:11, "*Mtakeni BWANA na nguvu zake…*"
- Mat. 26:41, "*Kesheni mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho I radhi lakini mwili ni dhaifu.*"
- Heb. 4:16, "*basin a tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Anaweza kuleta amani na furaha kwa waumini.

- Zaburi 29:11, "*BWANA atawapa watu wake nguvu; BWANA atawabariki watu wake kwa amani.*"

- Yoh. 14:27, "*Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi si kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu wala msiwe na woga.*"
- Yoh. 16:33, "*Hayo nimewambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo mimi nimeushinda ulimwengu.*

Amani ya Mungu inatokana na kufahamu kwamba yuko pamoja nasi bila kujali kile kinachotuangusha; na kwamba kuna maisha mazuri yajayo.

Tunamtafuta Mungu kwa sababu anauwezo wa uzima wa milele.

- Yoh. 1:12, "*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu., ndiyo wale waliaminio jina lake;*"
- Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"
- Yoh. 10:10, "*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*"

Kama tukimwamini, na kufanya mapenzi yake, tutakuwa na uzima wa milele – ameahidi hili. Hili ni kubwa kuliko kitu kingine ambacho tunaweza kukifikiria kwamba ulimwengu unaweza kutoa. Ebu fikiria katika fikra zako za ndani ya kitu utakachopenda katika ulimwengu huu. Karama ya Mungu kwako ni kubwa kuliko hiyo.

Yoh. 14:1-3, "*Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali nitakuja niwakaribishe kwangu ili nilipo mimi nanyi mwepo.*"

Lakini lazima tumtafute sasa, kabla hatujatarajia kuwa naye baada ya hapa.

Jinsi tunavyoweza kumuhitaji

Kwa mioyo yetu yote.

Luka 10:27, "*Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nasi.*"

Mioyo yetu haitakiwi kugawanyika. Tunapaswa kumweka juu ya kila kitu katika maisha yetu, pamoja na marafiki zetu, wenza wetu, na watoto wetu.

Mat. 10:35-38, "*…nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake. Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili, wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili. Wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili hanistahili.*"

Hii haimanishi kwamba tusiwapende – inamanisha hatupaswi kuwaweka juu ya upendo wetu na wajibu wetu kwa Mungu. Mara nyingi hapo nyuma nimewasikia wengine wanasema kwamba hawajaenda kanisani kwa sababu walikuwa na ndugu wanaotoka nje ya mji, na wakaa nyumbani ili kujifurahisha. Waombe waje, na kama hawapendi kuja, wambie utawaona baada ya kutoka kanisani. Mungu ni lazima awe muhimu katika maisha yetu.

Wengine wanajaribu kuishi katika ulimwengu mbili tofauti, lakini hiyo haiwafanyi wawe na furaha.

Jumapili, wanaishi maisha ya Ukristo; na siku zingine, wanaishi maisha na kidunia. Hawawezi kuridhika kwa maisha ya aina hiyo, na Mungu hawezi kufurahia.

Ulimwengu huu hauna chochote ambacho tunaweza kufaidika milele.

- Rum. 12:1-2, "*Basi ndugu zangu nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"
- Ufu. 3:15-16, "*Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto, nitakutapika utoke katika kinywa change. Basi kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa change.*"

Je tunahitaji kumpata Mungu?

Swali ni, "Ni kiasi gani tunamhitaji Mungu?"

Je tunahitaji la kutosha kuachia dhambi zetu na ubinafsi? Je tuko tayari kuachaa tofauti zetu?

Watu wengine wana ugomvi wao wenyewe:

- Wanamhitaji – vilevile hawataki.
- Wanahitaji njia yake – na wanahitaji njia zao pia.
- Wanataka wafanywe wapya – na wanahitaji kuwa tayari kuwa wachafu, pia.
- Hawatampata ikiwa bado wanaegemea duniani. Je ni kweli wanataka kumpata?

Je anafaa kutafutwa? Ndiyo!

Alituumba, na anatupenda. Alimtuma mwanaye kufa kwa ajili.

- Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"
- Efe. 5:2, "*Mkaenende katika upendo, kama Kristo naye alivyowapenda ninyi tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato.*"

- 1 Yoh. 4:16, "*Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi na kuliamini. Mungu ni pendo naye akaaye katika pendo hukaa ndaani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.*"

Anataka kutuokoa na kutupatia mbingu. Yoh. 14:1-3, "*Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*"

Hitimisho

Ninawezaje kumpata Mungu?

Maswali mengine mawili ni lazima yajibiwe kwanza:

- "Je ninahakika ninamhitaji?"
- "Je niko tayari kuacha kila kitu kinacho tungenganisha (dhambi)?" Anakutafta – acha akutafute – mgeukie!

Rum. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Imani. Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Toba. Mdo. 17:30, "*Basi zama zile za ujinga Mungu alijifanya kama haazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watu.*"

Kukiri. Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu*."

Ubatizo.

- Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"
- Yoh. 3:5, "*Yesu akajibu amini, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"
- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jinaa lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Mdo. 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"